



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 27-29 74369
Fax : 27- 29 74368
Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
HAI KILIMANJARO

Kumb.Na.LG/B.20/2/134

Tarehe: 30/11/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa kushirikiana na Divisioni ya afya, Ustawi wa Jamii na Lishe anawakaribisha wananchi wenye sifa kufanya maombi ya Ajira za Mkatoba katika Hospitali ya Wilaya ya Hai kwa kada zifuatazo;

1. MTEKNOLOJIA MSAIDIZI DAWA (3)

Sifa za mwombaji:

- i. Awe amehitimu astashahada ya mteknolojia msaidizi wa dawa kwa miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na ambae amesajiliwa.
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne (IV)

Majukumu na kazi

- i. Kuandaa mahitaji na matumizi ya dawa na vifaa
- ii. Kuagiza, kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
- iii. Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
- iv. Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MSHAHARA: Mshahara ni makubaliano.

Ujuzi/Job Skills: Awe na uwezo wa kutumia komputa.

2. MSAIDIZI WA HESABU (NAFASI 3)

Sifa za mwombaji:

i. Kuajiriwa wenye Cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali au Cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa zingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

ii. Awe na elimu ya kidato cha nne

Kazi na majukumu

- i. Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za uhasibu;
- ii. Kufanya usahili (bank reconciliation) wa kibenki.
- iii. Kutunza Kumbukumbu za hesabu;
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki; na
- v. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

MSHAHARA; Mshahara ni makubaliano.

2. MSAIDIZI MTEKNOLOJIA TEHAMA (NAFASI (1)

Sifa za mwombaji

- i. Awe na cheti cha elimu ya kidato cha nne.
- ii. Kuajiriwa wenye Cheti cha Astashahada ya TEHAMA kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.
- iii. Awe na uzoefu wa kutumia mifumo ya TEHAMA

Kazi na Majukumu

- i. Kupitia Sera za TEHEMA kwa ajili ya maboresho yake
- ii. Kusimika miundombinu ya TEHAMA pamoja na kusimamia matengenezo yake.

- iii. Kutoa mafunzo juu ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA.
- iv. Kushauri matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA na kusimamia manunuzi ya vifaa hivyo(hardware&software)
- v.Kutoa msaada wa kitaalam kwenye matumizi ya vifaa na mifumo ya TEHAMA.
- vi.Kushauri juu ya usimikaji wa mifumo mipya ya TEHAMA.
- vii.Kukusanya takwimu na taarifa za Hospitali ili na kuziweka kwenye mfumo (kanzidata)

MSHAHARA; Mshahara ni makubaliano.

NAMNA YA KUOMBA

Maombi yote yaambatanishwe na;

1. Maelezo binafsi (Curriculum vitae)
2. Vyeti vilivyo thibitishwa (Certified Certificates)
- 3.Cheti cha taaluma pamoja na cheti cha mafunzo kwa vitendo
- 4.Lesseni za taaluma
5. Cheti cha sekondari (kidato cha iv na kidato cha vi)
6. Cheti cha kuzaliwa
- 7.Kitambulisho cha NIDA/ Namba ya NIDA

MASHARTI KWA UJUMLA:

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe na Umri wa miaka 18 hadi 45.
3. Awe mwadilifu na asiwe na historia ya uhalifu
4. Waombaji waambatishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na wakili au mahakama
5. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo yakidato cha nne na sita (Form IV na Form VI result slip) havitakubalika.
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho kutoka mamlaka husika (TCU) wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.

7. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
8. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV)

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
HAI KILIMANJARO

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **31/12/2022** saa tisa na nusu alasiri
(9:30)

NB: Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.haidc.go.tz,
tovuti ya secretarieti ya ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za
Halmashauri.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-



Dionis M. Myinga
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
HAI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HAI**